

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S. L.P 30261

Kibaha.

Simu: (023) 2402658

Nukushi: (023) 2402657

Baruapepe: rbcpwani@pccb.go.tz

Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA WANANCHI KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

PWANI 04 JUNI, 2020

**TAKUKURU MKOA WA PWANI YAOKOA FEDHA ZA WAKULIMA SHILINGI
MILIONI HAMSINI NA MBILI (52,000,000/=) KUTOKA KWA WAFANYABIASHARA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Pwani imeokoa kiasi cha **shilingi Milioni hamsini na mbili (52,000,000/=)** za wakulima wa korosho wa chama cha Ushirika **JUHUDI AMCOS** wilaya ya kibiti kutokana na mauzo ya korosho za msimu wa mwaka 2019/2020.

Awali ilidaiwa kwamba wakulima hao waliuza korosho jumla ya **kg 65,000** (elfu sitini na tano) zenye thamani ya **Shilingi 52,000,000/=** kwa kampuni ya **CDJKL NUTS** ambayo iliingia mkataba wa kununua korosho za wakulima hao siku ya tarehe **16 Machi 2020** kwa makubaliano kwamba watalipa fedha baada ya mwezi mmoja.

Aidha kampuni hiyo ya **CDKJL NUTS** haikutekeleza makubaliano yaliyoainishwa katika mkataba ya kulipa fedha kwa wakati, badala yake kampuni hiyo ikaaanza kuwasumbua wakulima kwa madai kuwa wanunuzi walionunua korosho hizo ambao wanaishi nchini India wako 'lock down' kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa **CORONA** yaani **COVID 19** hivyo kwa sasa hawawezi kulipa fedha hizo mpaka ugonjwa huu utakapoisha.

Ofisi ya **TAKUKURU (W)** Kibiti ilipokea malalamiko hayo kutoka kwa wakulima wa chama hicho na katika uchunguzi wake ilibaini kwamba, ni kweli kampuni hiyo iliingia mkataba na wakulima bila kuushirikisha uongozi wa wilaya kwa lengo la kuwalaghai kwani hata bei waliyonunulia sio bei iliyokuwa imekubaliwa kwenye mnada.

Hivyo ofisi ilichukua hatua na kuhakikisha wanunuzi hao wanalipa fedha za wakulima ndani ya siku saba, huku wakipewa onyo kuwa wasipotekeleza maagizo hayo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ikiwa ni pamoja na kuwazuia kutojihusisha (blacklisting) na biashara ya mazao katika wilaya ya Kibiti.

Kwa juhudi hizo za TAKUKURU tayari fedha hizo za wakulima zimeshalipwa jumla ya Shilingi **52,000,000/= (Milioni hamsini na mbili)** na taratibu za kuziwasilisha fedha hizo kwa wananchi zinaendelea.

WITO

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Bi SUZANA RAYMOND anawaasa wafanyabiashara au makampuni yanayofanya biashara za mazao katika mkoa wa Pwani wafuate sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali ili kuepusha malalamiko kwa wananchi, kwani wakulima wanahangaika sana kuzalisha wakitegemea kupata mazao bora yatakayowaondoa katika wimbi la umasikini. Tufuate mtazamo wa Mhe Rais wetu katika kumsaidia mkulima ili aone matunda ya kazi zake.

KATAA RUSHWA JENGA NCHI YAKO

Imetolewa na:

SUZANA RAYMOND,

MKUU WA TAKUKURU MKOA WA PWANI